

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI

Simu: +255262963470  
Nukushi: +255262963117  
Barua pepe: [ps@mit.go.tz](mailto:ps@mit.go.tz)  
Tovuti: [www.mit.go.tz](http://www.mit.go.tz)



Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM),  
Kitivo cha Sanaa, Sayansi  
ya Jamii, na Maendeleo,  
Ghorofa ya 1, Jengo Na. 12,  
S. L. P 2996, DODOMA.

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

Kati ya tarehe 13 na 14 Novemba 2018, Mhe. Joseph G. Kakunda (MB), Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji (WVBU), alifanya ziara ya kikazi katika Mikoa ya Lindi na Mtwara. Akiwa katika maeneo hayo, Mhe. Waziri alijionea ufanisi duni wa mfumo wa maghala uliochangia kuzorotesha soko na bei ya zao la korosho. Mhe. Waziri alijiridhisha kuwa hali hiyo imesababishwa na utendaji kazi hafifu, uzembe, na usimamizi duni wa Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) Tanzania.

Kutokana na hali hiyo, na kwa Mamlaka aliyonayo kwa mujibu wa Kifungu Na.7(1) cha Sheria Na.10 ya mwaka 2005 ya Stakabadhi za Maghala Sura ya 339 na marekebisho yake ya mwaka 2016 ikisomwa sambamba na Kifungu Na.48(1)(a) cha Sheria ya Tafsiri Sura Na.1, leo tarehe 15 Novemba 2018, Mhe. Waziri ametengua uteuzi wa Bw. Augustino W. Mbulumi, Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB). Bw. Mbulumi atapangiwa kazi nyingine.

IMETOLEWA NA

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Jhonde'.

Kitengo cha Habari na Mawasiliano Serikalini  
Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji (WVBU)  
15 Novemba 2018